

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ufafanuzi Kuhusu Uhusiano Kati ya Ukuaji wa Pato la Taifa, Ujazi wa Fedha na Mfumuko wa Bei 30 Oktoba 2017

Tunapenda kukanusha taarifa ziliyotolewa hivi karibuni na Mhe. Zitto Kabwe (Mb) kuwa takwimu za pato la taifa, ujazi wa fedha na mfumuko wa bei zinatia mashaka. Mhe. Kabwe amesema kuwa ukuaji wa pato la taifa kwenye robo iliyoishia Juni mwaka 2017 ulipaswa kuwa asilimia 0.1 na siyo asilimia 5.7 kama ilivyochapishwa katika ripoti ya robo mwaka ya Benki Kuu, kauli ambayo si sahihi.

Ukuaji wa asilimia 5.7 alioutaja Mhe. Kabwe ulikuwa wa robo ya kwanza ya mwaka 2017 na siyo robo ya pili. Ripoti ya Benki Kuu aliyoitumia ilikuwa na takwimu za hadi robo ya kwanza ya mwaka 2017, kwani ilichapishwa kabla takwimu za pato la taifa za robo ya pili hazijatolewa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa. Ukuaji wa pato halisi la taifa katika robo ya pili ya mwaka 2017 ulikuwa asilimia 7.8.

Mhe. Kabwe amekokotoa ukuaji wa pato la taifa anaodai kuwa sahihi, kwa kuangalia tofauti kati ya ongezeko la ujazi wa fedha (m) na mfumuko wa bei (p) kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali 1**.

Jedwali 1: Ukuaji wa Pato la Taifa Uliokokotolewa

Kiashiria	Kiasi	Mwaka unaoishia
A. Ongezeko la ujazi wa fedha (m)	6.1	Robo ya pili ya 2017
B. Mfumuko wa bei (p)	6.0	Robo ya pili ya 2017
C. Ukuaji wa GDP (y^*) (A-B)	0.1	Robo ya kwanza ya 2017 ¹

Ukokotoaji wa aina hii umejengwa juu ya nadharia inayoitwa *quantity theory of money* ambayo kimsingi inasema mfumuko wa bei hutokea pale fedha zinapongezeka kwa kasi zaidi kuliko uzalishaji wa vitu halisi. Katika nadharia hii ongezeko “sahihi” la ujazi wa fedha (m) linaweza kukokotolewa kama ifuatavyo:

$$m = p + y \quad \text{endapo kasi ya mzunguko wa fedha (velocity of money circulation (v)) haibadiliki.}$$

¹ Amelinganisha jawabu hili na ukuaji wa asilimia 5.7 wa robo ya kwanza ya mwaka 2017

Maana yake, ukuaji wa fedha (m) unapaswa kuwa sawa na mfumuko wa bei (p) jumlisha ukuaji halisi wa uchumi (y). Hata hivyo ni muhimu kuzingatia kuwa mfumuko wa bei unaotumika katika kanuni hii sio ule unaotokana na fahirisi ya bei ya walaji (*consumer price index*) bali ni ule unaotokana na fahirisi ya pato la taifa (*GDP deflator*).

Kutokana na nadharia hii tunaweza kusema kuwa ukuaji wa uchumi ni sawa na tofauti kati ya ukuaji wa fedha na mfumuko wa bei.

$$y = m - p$$

Mhe. Kabwe ametumia m na p za robo ya pili ya mwaka 2017 akapata 0.1 (yaani $6.1 - 6.0 = 0.1$) na hivyo akahitimisha kwa kusema kuwa ukuaji wa pato la taifa wa asilimia 5.7 ulio kwenye ripoti ya Benki Kuu unatia mashaka.

Ni vyema ieleweke kuwa, si sahihi kutumia nadharia ya *quantity theory of money* kuelezea mwenendo wa fedha, mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi katika kipindi cha muda mfupi kama Mhe. Kabwe alivyofanya.

Pamoja na hayo tunapenda kuainisha vipengele kadhaa muhimu ambavyo Mhe. Kabwe alitakiwa kuvizingatia katika kufikia uamuzi wa kusema kuwa ukuaji wa uchumi ulipaswa kuwa asilimia 0.1.

Kwanza: uhusiano kati ya takwimu za uchumi hautarajiwi kuwa wa moja-kwa-moja kila wakati. Madai yake yanamaanisha kuwa, kama ongezeko la ujazi wa fedha likipungua katika robo ya pili ya mwaka 2017, basi na ukuaji wa pato la taifa nao unapaswa kupungua katika robo hiyohiyo ya mwaka. Hali halisi huwa haiko hivyo. Kwa mfano: mikopo inaweza kuongezeka kipindi hiki kwa ajili ya miradi mikubwa ya uzalishaji lakini ongezeko la tija likatokea kwenye kipindi kijacho baada ya miradi hiyo kukamilika, bila mikopo kuongezeka katika kipindi hicho. Hii ni kawaida kabisa katika mahusiano ya takwimu za uchumi.

Pili: kanuni aliyoitumia haikuweka uzito kwenye kipengele muhimu cha kasi ya mzunguko wa fedha (*velocity of money circulation* (v)). Fedha inapozunguka kwa kasi kubwa inaweza kutosheleza kwa shughuli nyingi za uchumi kuliko inapozunguka kwa kasi ndogo. Katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia mabadiliko makubwa ya kiteknolojia ambayo yamepunguza gharama na ugumu wa kufanya miamala ya fedha. Hii inafanya malipo yafanyike kwa wepesi na haraka zaidi jambo ambalo linaongeza

kasi ya kuzunguka kwa fedha na hivyo kufanya fedha kidogo itoshe kwa shughuli nyingi zaidi za uchumi.

Ili kufafanua jinsi kasi ya mzunguko wa fedha inavyobadili uhusiano kati ya fedha, mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi tutumie mfano rahisi: basi moja la abiria likifanya safari kumi kwa siku linabeba abiria wengi zaidi kuliko likifanya safari tano. Katika mfano huu ni bayana kuwa, ukiwa na mabasi yanayofanya safari kumi kwa siku unahitaji mabasi machache zaidi kuhudimia abiria walewale, kuliko ukiwa na mabasi yanayofanya safari tano tu kwa siku. Vivyo hivyo, fedha zinapozunguka kwa kasi kubwa zinahitajika chache zaidi kutosheleza kiwango kilekile cha shughuli za uchumi kuliko zikiwa zinazunguka kwa kasi ndogo.

Kwa sababu hii ni muhimu kuweka kasi ya mzunguko wa fedha katika kanuni ya kukokotoa ukuaji “sahih” wa uchumi kama ifuatavyo:

$$y = m - p + v$$

ambapo v ni ongezeko la kasi ya mzunguko wa fedha.

Kama kasi ya mzunguko wa fedha inaongezeka ina maana kuwa v itafanya y iwe kubwa kuliko $m - p$. Mhe. Kabwe ameweka uzito mdogo kwenye v na hivyo kufanya isiwe na mchango katika kupata y . Kutokuweka uzito kwenye v kunaweza kusababisha sera ya fedha ikawa na matokeo mabaya kwa sababu kama mzunguko wa fedha unaongezeka, na sera ya fedha ikaendelea bila kuzingatia jambo hilo, matokeo yake yatakuwa mfumuko mkubwa wa bei badala ya ongezeko katika ukuaji wa uchumi.

Tatu: hata kama tukizingatia uhusiano wa kuchelewa (*lags*) kati ya takwimu za kiuchumi, bado hali halisi ya uchumi haitarajiwi kuendana na nadharia kila wakati na kila mahali. Kwa kawaida nadharia hueleza kiasi fulani cha uhusiano katika takwimu halisi. Kuna mambo mengi mengine yanayotokea ambayo hayamo katika nadharia ya *quantity theory of money* lakini yana uwezo wa kusababisha kasi ya ukuaji wa uchumi ikaongezeka. Baadhi ya mambo hayo ni haya yafuatayo:


- i. Kukamilika kwa miradi mikubwa kunaongeza uzalishaji hata kama hakuna ongezeko la fedha au mikopo
- ii. Kupungua kwa gharama za uzalishaji kutokana na kupungua kwa bei ya nishati na kuwepo kwa umeme wa kutosha kwenye gridi ya taifa
- iii. Kuongezeka kwa ufanisi katika uzalishaji mfano kusafirisha gesi kwenye bomba na mabadiliko ya teknolojia

- iv. Kupungua kwa vikwazo vya biashara mipakani mwa nchi
- v. Hali nzuri ya hewa n.k.

Nne: Kama tulivyotangulia kusema Mhe. Kabwe amepotosha kwa kutumia fahirisi ya bei ya walaji (CPI) kukokotoa ukuaji “sahihi” wa pato la taifa badala ya kutumia fahirisi ya pato la taifa (*GDP deflator*). Pamoja na kuwa fahirisi hizi zinapaswa kuendana kama zikiangaliwa kwa kipindi kirefu (*in the long-run*), zinaweza kutofautiana sana katika kipindi cha muda mfupi (*in the short-run*). Hivyo ni makosa kuhoji usahihi wa takwimu rasmi kwa kutumia ukokotoaji ambao una kasoro.

Tano: hata kama kanuni aliyotumia Mhe. Kabwe ingekuwa sahihi, si mara ya kwanza tofauti kati ya ukuaji aliopata kuwa kubwa kama alivyosema. **Kielelezo 1.** kinaonyesha kuwa tofauti hiyo ilikuwa kubwa kushinda mwaka huu katika miaka ya 2006, 2008, 2011 na 2012 (tofauti ya robo ya kwanza imeonyeshwa kwa rangi iliyokolea zaidi). Hivyo si sahihi kusema kuwa mwenendo kama huu haukuwahi kutokea. Takwimu halisi zinaweza kusomwa kwenye **Jedwali 2.**

Kielelezo 1: Tofauti ya Ukuaji wa Uchumi Uliokokotolewa kwa Kanuni Aliyoitumia Mhe. Kabwe na Ulioripotiwa na NBS ($y^* - y$)



Hitimisho

Tunapenda tena kukanusha taarifa iliyotolewa na Mhe. Kabwe kwamba takwimu zilizotolewa kwenye taarifa ya robo mwaka ya Benki Kuu zinatia mashaka na kuwaomba wananchi kwa ujumla wazipuuze.

Jedwali 2: Uhusiano kati ya Ujazi wa Fedha, Mfumuko wa Bei na Ukuaji wa Pato la taifa

A Mwaka	B Robo	C Mfumuko wa bei (p)	D Ongezeko la fedha M3 (m)	E Ukuaji wa pato la taifa ilivyoripotiwa na NBS (y)	F Ukuaji wa pato la taifa uliokokotolewa (y*-m-p)	G Totauti (y*-y)
2006	Q1	7.7	30.9	3.3	23.2	19.9
	Q2	9.2	31.3	4.7	22.1	17.5
	Q3	5.9	28.6	5.7	22.7	16.9
	Q4	6.3	21.5	4.6	15.2	10.6
2007	Q1	7.2	19.0	10.9	11.8	0.9
	Q2	5.7	20.1	6.8	14.4	7.6
	Q3	8.4	18.1	6.6	9.8	3.2
	Q4	6.9	20.5	9.6	13.6	3.9
2008	Q1	8.9	25.2	3.8	16.4	12.6
	Q2	9.4	18.1	5.0	8.7	3.7
	Q3	10.3	21.2	9.7	10.9	1.2
	Q4	12.5	19.8	3.9	7.3	3.4
2009	Q1	13.1	14.3	6.8	1.3	-5.5
	Q2	11.3	18.5	3.0	7.1	4.1
	Q3	11.7	19.0	2.6	7.3	4.8
	Q4	12.5	17.7	9.3	5.3	-4.0
2010	Q1	13.1	18.9	5.0	5.8	0.8
	Q2	8.2	25.1	7.4	16.9	9.6
	Q3	5.8	22.6	5.1	16.8	11.7
	Q4	6.5	25.4	8.0	18.9	10.9
2011	Q1	7.3	23.8	8.0	16.5	8.5
	Q2	9.7	22.0	10.3	12.3	2.1
	Q3	14.6	23.7	9.3	9.1	-0.2
	Q4	18.9	18.2	4.4	-0.7	-5.1
2012	Q1	19.4	15.7	7.0	-3.6	-10.6
	Q2	18.1	10.9	3.4	-7.2	-10.6
	Q3	14.7	9.5	5.5	-5.2	-10.7
	Q4	12.4	12.5	4.7	0.1	-4.5
2013	Q1	10.4	14.0	6.8	3.6	-3.1
	Q2	8.4	14.9	6.3	6.5	0.2
	Q3	6.8	13.6	7.2	6.9	-0.4
	Q4	6.0	10.0	8.7	3.9	-4.8
2014	Q1	6.0	11.6	7.8	5.6	-2.2
	Q2	6.4	15.8	9.8	9.4	-0.4
	Q3	6.6	14.7	5.7	8.1	2.4
	Q4	5.5	15.6	4.4	10.1	5.6
2015	Q1	4.2	13.2	6.5	9.1	2.6
	Q2	5.3	13.1	6.5	7.8	1.3
	Q3	6.3	16.5	6.8	10.2	3.3
	Q4	6.6	18.8	8.2	12.2	4.1
2016	Q1	5.8	15.5	6.9	9.7	2.8
	Q2	5.3	12.7	8.5	7.5	-1.0
	Q3	4.8	4.7	7.0	-0.1	-7.1
	Q4	4.8	3.4	5.5	-1.3	-6.8
2017	Q1	5.7	4.6	5.7	-1.1	-6.8
	Q2	6.0	6.1	7.8	0.1	-7.7